OFISI YA MWANASHERIA
MKUU WA SERIKALI

# OAG

# WIKI HII
*KWENYE*
# MAGAZETI
*NA*
MITANDAONI

oagtanzania

www.oag.go.tz

HABARI KITA

# Wagombea vijana TLS kupambana na vishoka

Na Pilly Kigome

WAGOMBEA nafasi ya urais na uenyekiti, mawakili vijana kutoka Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS), wamejinadi kurudisha chama hicho kuwa na nguvu ya awali kwa kutimiza misingi halali ya uchaguzi na kuondokana na vishoka katika taaluma hiyo.

Baadhi ya wagombea wa nafasi ya urais TLS, walisema hayo walipokuwa wakizungumza na waandishi wa habari makao makuu ya ofisi hizo jijini Dar es Salaam baada ya kumalizika kwa mdahalo uliowakutanisha wagombea hao.

Wakili Revocatus Kuuli, alisema kuna baadhi ya watu wanakiona chama hicho kupoteza ubora, lakini wagombea ambao tunagombea sasa tumeweka mikakati ya kukirudisha chama kuwa na nguvu na kutekeleza misingi iliyojiwekea chama.

Alisema chama kikipoteza misingi na kukosa watu makini, lazima kitayumba na dhamira ya wagombea wajao ni kukirudisha kiwe katika misingi imara.

Naye Wakili Sweetbert Nkuba, alisema kama atapata dhamana ya kukiongoza chama hicho atahakikisha atasambaratisha vishoka walioko kwenye taaluma hiyo ambao hawajasomea sheria.

Alifafanua atahakikisha mawakili wote wanasajiliwa katika chama ili kugundua wababaishaji kwa kutaka kutambua waliposajiliwa, ofisi zao zitambulike kisheria ili kuwabaini wale wababaishaji wasio na ofisi wazuiwe wasifanye kazi za uwakili.

"Kuna baadhi ya watu wanaojiita mawakili wanafanyia kazi zao za uwakili hata baa, sasa hao mimi nikipata dhamana tutacheza nao kwa maana wanaharibu taaluma," alisema.

Alisema kuimarisha TLS kunatakiwa kuwe na sauti moja ambayo kitaimarisha chama na ikiwamo na kupatikana viongozi wenye umakini na dhamira thabiti ya kusimamisha chama na si ujanja ujanja.

Aidha, alisema akipata dhamana atahakikisha anasaidia mawakili vijana chipukizi wasitozwe ada nyingi kuwa mawakili, kuwajengea weledi kwa kuwa mawakili wengi wanashindwa kutekeleza kazi zao kwa kukosa mitaji na maeneo ya kufanyia kazi.

"Nitahakikisha kupatikana kwa maslahi ya mawakili, bima ya afya na bima ya maisha kwa mawakili, vituo vya malezi kwa mawakili vijana pamoja na kuboresha mahusiano na kuunganisha mawakili na taasisi muhimu za serikali ikiwamo mahakama na jamii," alifafanua.

Naye mgombea wa nafasi ya uenyekiti wa mawakili vijana, wakili Denis Bwana alisema kwa kupitia Sheria namba 307 ya Bunge katika kifungu cha nne, TLS ina wajibu kuishauri serikali, kuishauri Bunge TLS kuwa ni chombo cha mfano katika jamii kwa kusaidia masuala ya kisheria nchini.

# Chinese legal firm opens office in Dar

**By Guardian Reporter**

China's Yingke Global One Hour Legal Service Ecosystem, a one-stop comprehensive service platform, on Saturday officially opened its office in Tanzania to provide clients with cross-regional, cross-language, cross-cultural, and interdisciplinary support.

The opening ceremony, held in the port city of Dar es Salaam, coincided with the Tanzania-China Economic and Investment Cooperation Reception, which aimed to deepen economic ties, promote sustainable development, and create mutually beneficial opportunities for both countries.

The ceremony, attended by delegations from the governments and private sectors of China and Tanzania, including over 20 companies from Tanzania and 13 companies from China, saw the signing of a memorandum of understanding by Tanzania Investment Center (TIC) Executive Director Gilead Teri and head of the Global Board of Directors of Yingke Law Firm, Mei Xiangrong.

Mei said Yingke Global One Hour Legal Service Ecosystem provides clients worldwide with professional services ranging from legal, accounting, taxation, consulting, investment and financing, mergers and acquisitions to agriculture, mining, cultural tourism, and science and technology.

"I am excited to work in Tanzania because Africa is the future, and China and Africa can work together to achieve robust economic growth," said Mei.

Teri said the Tanzania-China Economic and Investment Cooperation Reception provided a platform for government officials, business leaders, and industry experts to engage in a dialogue about policy reforms and regulatory frameworks that can improve the business environment and attract more foreign investment, especially from China.

# Hatima Wakili Mwabukusi kugombea TLS Ijumaa

James Magai, Mwananchi
jmagai@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Hatima ya Wakili Boniface Mwabukusi kugombea urais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) itajulikana keshokutwa Ijumaa, wakati Mahakama Kuu itakapotoa uamuzi wa shauri lake la kupinga kuenguliwa katika kinyang'anyiro hicho.

Uamuzi huo unaotarajiwa kutolewa siku hiyo na Jaji Butamo Phillip, ndio utaamua hatima ya Mwabukusi katika kinyang'anyiro hicho.

Mwabukusi alikuwa mmoja wa wanachama walioomba na kupitishwa na Kamati ya Uchaguzi kugombea nafasi ya urais wa TLS, unaotarajiwa kufanyika Agosti 2, 2024 jijini Dodoma, lakini aliondolewa katika kinyang'anyiro hicho na Kamati ya Rufaa ya Uchaguzi baada ya kusikiliza rufaa iliyokatwa dhidi yake.

Katibu wa Kamati Uchaguzi wa TLS, ambaye pia ni katibu wa Kamati ya Rufaa ya Uchaguzi TLS, Nelson Frank alilieleza *Mwananchi* kuwa Mwabukusi aliondolewa katika kinyang'anyiro hicho baada ya kamati hiyo kujiridhisha hana sifa kwa mujibu wa kanuni.

"Mwabukusi anakosa sifa moja katika kanuni ya 13 (c) kwa sababu alishatiwa hatiani kwenye Kamati ya Maadili, akapewa adhabu ya onyo na hiyo hukumu bado haijatenguliwa, hivyo bado ana doa la kimaadili kinyume na kanuni hiyo ya 13.

Hata hivyo, Mwabukusi hakukubaliana na uamuzi huo, hivyo alifungua shauri la maombi Mahakama Kuu Dar es Salaam, akaomba ridhaa ya kupinga uamuzi huo kwa njia ya shauri la maombi ya mapitio ya mahakama na amri ya zuio la muda la uchaguzi huo.

Mahakama katika uamuzi wake uliotolewa Julai 17, 2024 na Jaji Salma Maghimbi aliyesikiliza maombi hayo, ilimkatalia ombi la amri ya zuio la muda la uchaguzi huo, lakini ikamruhusu kufungua shauri la maombi ya mapitio ya mahakama, kupinga kuenguliwa kwake ndani ya siku 14.

Akizungumza na *Mwananchi* jana, Mwabukusi alisema baada ya kupata ridhaa hiyo tayari alishafungua shauri hilo na kwamba lilishasikilizwa na mahakama imepanga kutoa uamuzi keshokutwa.

"Nimeshafungua na kusikilizwa na Jaji Phillip, uamuzi unakuja Ijumaa hii ya tarehe 25, saa tatu asubuhi," alisema Mwabukusi.

Mmoja wa mawakili wa Mwabukusi, Edward Heche alilieleza *Mwananchi* shauri hilo lilishafunguliwa tangu siku ya shauri la maombi ya ridhaa lilipokililizwa na kuamuriwa, Julai 17 na kwamba shauri hilo la mapitio lilisikilizwa juzi.

Mbali na Heche, Mwabukusi anawakilishwa na jopo la mawakili 29, linaloongozwa na Mpale Mpoki. Mawakili wengine baadhi yao ni Peter Kibatala, Jebra Kambole, Dickson Matata, Aziza Msangi na Happiness Michael.

Katika shauri hilo, Mwabukusi na wengineo anaiomba mahakama itoe amri ya kutengua uamuzi wa Kamati ya Rufaa ya Uchaguzi wa TLS, pamoja na mambo mengine akidai kuwa unakiuka misingi ya kanuni ya haki asili kwa kuenguliwa bila kumpa haki ya fursa ya kusikilizwa.

Iwapo mahakama itakubaliana na hoja zake za kupinga kuenguliwa kuwa sababu za kumuengua hazikuwa halali, basi mahakama hiyo kupitia uamuzi huo itatoa amri ya kurejeshwa katika kinyang'anyiro hicho kwenda kuchuana na wagombea wengine wa nafasi hiyo.

Wagombea wengine wa nafasi hiyo ya urais wa TLS ni makamu wa rais wa zamani wa TLS, Ibrahim Bendera, Revocatus Kuuli, Emmanuel Muga, Sweetbert Nkuba na Paul Kaunda.

**HOJA**

**Mwabukusi anaiomba mahakama itoe amri ya kutengua uamuzi wa Kamati ya Rufaa ya Uchaguzi wa TLS, pamoja na mambo mengine akidai kuwa unakiuka misingi ya kanuni ya haki asili kwa kuenguliwa bila kumpa haki ya fursa ya kusikilizwa.**

**Iwapo mahakama itakubaliana na hoja zake za kupinga kuenguliwa kuwa sababu za kumuengua hazikuwa halali, basi mahakama hiyo kupitia uamuzi huo itatoa amri ya kurejeshwa katika kinyang'anyiro hicho kwenda kuchuana na wagombea wengine wa nafasi hiyo.**



**OAG Tanzania**
1d ·

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yatunukiwa Cheti cha heshima kwa mchango wake katika kufanikisha Kikao cha 77 cha Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu.

See translation


Cheti cha Pongezi

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Tunatambua na kuheshimu huduma uliyotoa katika kufanikisha Kikao cha 77 cha Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kilichofanyika kuanzia tarehe 20 Oktoba hadi 09 Novemba, 2023 katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC)

Mhe. Balozi Dkt. Pindi H. Chana — WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA — SJMT

Mhe. Haroun Ali Suleiman — WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS KATIBA SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA — SMZ

1

**OAG Tanzania**
12h ·

Matukio ya Maadhimisho ya Kumbukumbu ya Siku ya Mashujaa, tarehe 25 Julai 2024, Dodoma.

See translation




Like Comment Send Share

**Nipashe Tanzania** @Nipashetz · 15h

Hukumu ya kesi hiyo kati ya Mwabukusi dhidi ya TLS, ipo Mahakama Kuu (Masijara Ndogo ya Dar es Salaam), mbele ya Jaji Butamo Kasuka Phillip./ippmedia.com/nipashe/habari…




2 423

**fullshangweblog**


Cheti cha Pongezi

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Tunatambua na kuheshimu huduma uliyotoa katika kufanikisha Kikao cha 77 cha Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kilichofanyika kuanzia tarehe 20 Oktoba hadi 09 Novemba, 2023 katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC)

Mhe. Balozi Dkt. Pindi H. Chana — WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA — SJMT

Mhe. Haroun Ali Suleiman — WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS KATIBA SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA — SMZ

2 likes

fullshangweblog Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yatunukiwa Cheti cha heshima kwa mchango wake katika kufanikisha Kikao cha Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu. @oagtanzania

**OAG Tanzania**

6h ·

DIVISHENI YA URATIBU NA USHAURI YAWAPIGA MSASA MAWAKILI WA SERIKALI

Divisheni ya Uratibu na Ushauri wa Kisheria imeratibu na kuendesha mafunzo ya kitaaluma kwa Mawakili wa Serikali, mafunzo hayo yamefanyika tarehe 26 Julai 2024, katika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu zilizoko Mtumba Jijini Dodoma.

Mada kuu katika mafunzo hayo ilihusu Uandishi wa Ushauri wa Kisheria, ambapo mada hiyo iliwasilishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi Bw. Ladislaus Komanya aliyeshirikia na Wakili wa Serikali Mkuu Bi Grace Komba.

Huu ni mwendelezo wa utoaji wa mafunzo ya kitaaluma kwa Mawakili wa Serikali unaofanywa na Divisheni ya Uratibu na Ushauri ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambapo hivi karibuni Divisheni hiyo iliendesha mafunzo kuhusiana na ushirikiano kikanda.

See translation

